# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**OFISI YA RAIS**

**MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA**

# KITINI CHA KUFUNDISHIA MWONGOZO WA KUDHIBITI VVU, UKIMWI NA MAGONJWA SUGU YASIYOAMBUKIZWA KATIKA UTUMISHI WA UMMA

**Kimetolewa na:**

Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma,

Aprili, 2015

DIBAJI

Kitini hiki ni kwa ajili ya kutoa elimu kwa watumishi wa umma juu ya VVU, UKIMWI na Magonjwa Sugu Yasiyoambukizwa (MSY) ambayo yanaathiri afya na ufanisi wa watumishi wa umma. Magonjwa haya huwapata siyo tu watu wenye kipato kikubwa bali hata wenye kipato cha chini na yanaongezeka kote mijini na vijijini. Baadhi ya magonjwa hayo ni pamoja na ugonjwa wa kisukari, shinikizo kubwa la damu, moyo, saratani na magonjwa sugu ya njia ya hewa. Takwimu zinaonesha kuwa asilimia 27 ya watanzania wana tatizo la shinikizo kubwa la damu na asilimia 9 wana tatizo la kisukari. Vilevile tafiti zinaonesha kuwa hadi asilimia 80 ya magonjwa ya moyo na kisukari; na zaidi ya asilimia 50 ya saratani yanaweza kuzuilika kwa kuwa na mtindo wa maisha unaozingatia ulaji unaofaa, mazoezi ya mwili, kuwa na uzito usiozidi kiasi kulingana na urefu na kuepuka matumizi ya pombe na sigara. (WHO/MoHSW STEPS Survey 2012).

Magonjwa haya yanahatarisha uhai, yana gharama kubwa za matibabu, yanapunguza mahudhurio kazini na tija ya wafanyakazi na ongezeko la gharama za mazishi. Hata hivyo mbinu za kuzuia magonjwa haya zinajulikana na zipo ndani ya uwezo wa mtu binafsi na gharama ni ndogo ikilinganishwa na gharama za matibabu. Pamoja na changamoto mpya ya MSY katika Utumishi wa Umma, VVU na UKIMWI vimeendelea kuwa ni tatizo kubwa mahali pa kazi. Juhudi zimechukuliwa na serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali katika kukabiliana na UKIMWI, ambazo zimesababisha kupungua kwa kiwango cha maambukizi ya VVU nchini kutoka asilimia 7 (THIS, 2004) hadi asilimia 5.1 Utafiti wa Kitaifa kuhusu UKIMWI na Malaria (THMIS 2012). Tafiti zimethibitisha kwamba maambukizi ya VVU yanaweza kuzuilika kwa zaidi ya asilimia 90 kwa kubadili mienendo na tabia hatarishi. Aidha, katika utafiti uliyofanywa na Shirika la Kazi Duniani kwenye Sekta ya Umma na Binafsi kuhusu unyanyapaa, takwimu zinaonesha kwamba asilimia 36 ya watumishi wanaoiishi na VVU walishindwa kuomba ruhusa ya kuhudhuria matibabu.

Kwa kuzingatia mchango wa Watumishi wa Umma kwa ustawi wa taifa, udhibiti wa magonjwa haya Mahali pa Kazi unapewa msukumo wa kipekee ili kunusuru afya zao na kuleta tija. Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma (OR-MUU) iliandaa Mwongozo unaoelekeza Wizara na taasisi zake, Idara zinazojitegemea, Sekretarieti za Mikoa, Wakala za Serikali na Mamlaka za Serikali za Mitaa, juu ya utaratibu madhubuti wa kudhibiti VVU, UKIMWI na MSY katika Utumishi wa Umma ambao umeandaliwa Kitini hiki cha mafunzo.

Mhe. Celina Ompeshi Kombani (Mb)
**Waziri wa Nchi - Ofisi ya Rais**
**Menejimenti ya Utumishi wa Umma**

## SHUKRANI

Kitini hiki cha kufundishia Mwongozo wa kudhibiti VVU, UKIMWI na MSY Mahali pa kazi ni matokeo ya weledi, ubunifu, ari kubwa na ushirikiano wa wadau mbalimbali. Utayarishaji na uchapishaji wa kitini hiki usingefanyika bila msaada wa wataalamu na Shirika la Kazi Duniani (ILO).

Watumishi na wataalamu wa Taasisi za Umma na Wadau wa Maendeleo walishiriki kwa njia mbalimbali kutoa taarifa mahususi, na ushauri wa kitaalamu kwa lengo la kuwezesha kitini hiki kukamilika.

Shukrani za pekee zinatolewa kwa watumishi wa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma kwa kuona umuhimu wa uwepo wa kitini hiki. Kimsingi kitini hiki kitasaidia kutoa mafunzo ya VVU, UKIMWI na MSY kwa watumishi wa Umma, yenye maudhui yanayofanana.

Aidha, ninatoa shukrani za dhati kwa taasisi zilizotoa wataalamu kuandaa kitini hiki kwa kushirikiana na watumishi wa ofisi yangu. Taasisi hizi ni pamoja na Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (PMO-RALG), Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS), Chuo cha Utumishi wa Umma (TPSC), na GIZ.

Mwisho, shukrani za pekee ziende kwa Taasisi nyingine ambazo hazikutajwa na zilishiriki kukamilisha kitini hiki.

HAB Mkwizu
**KAIMU KATIBU MKUU (UTUMISHI)**

## ORODHA YA VIFUPISHO VYA MANENO

| | | |
|---|---|---|
| AIDS | - | Acquired Immuno-Deficiency Syndrome |
| ARVs | - | Anti- Retro Viral - (Dawa za kufubaza makali ya VVU) |
| BMI | - | Body Mass Index |
| CD4 | - | Cluster of Differentition 4 (Seli katika damu zinazohusika na kinga ya mwili ikiwa ni pamoja na kushambulia VVU) |
| GIZ | - | German International Cooperation |
| ILO | - | International Labour Organization (Shirika la Kazi Duniani) |
| LGAs | - | Local Government Authorities |
| MDAs | - | Ministries, Departments and Agencies |
| MoHSW | - | Ministry of Health and Social Welfare |
| MSY | - | Magonjwa Sugu Yasiyoambukizwa |
| OR-MUU | - | Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma |
| PMO-RALG | - | Prime Minister’s Office, Regional Administration and Local Government |
| PO-PSM | - | President’s Office, Public Service Management |
| RS | - | Regional Secretariat |
| TACAIDS | - | Tanzania Commission for AIDS |
| THMIS | - | Tanzania HIV/AIDS and Malaria Indicator Survey |
| UKIMWI | - | Ukosefu wa Kinga Mwilini |
| VVU | - | Virusi vya UKIMWI |
| WAVIU | - | Watu wanaoishi na VVU |
| WHO | - | World Health Organisation |

## YALIYOMO:

**1.0 Sehemu A ......................................................................... Ukurasa 8**
1.1 Utangulizi ......................................................................... –“-
1.2 Madhumuni ......................................................................... –“-
1.3 Mbinu za uwezeshaji ......................................................................... –“-
1.4 Vifaa vitakavyotumika ......................................................................... –“-
1.5 Muda wa mafunzo ......................................................................... Ukurasa 9

**2.0 Sehemu B ......................................................................... Ukurasa 10**

2.1 **Mada ya Kwanza:** Umuhimu wa kudhibiti VVU na UKIMWI katika Utumishi wa Umma **.............................. Ukurasa 10**
2.1.1 Malengo Mahususi: ........................................... –“-
2.1.2 Maudhui ........................................... –“-
2.1.3 Shughuli Mahususi ........................................... –“-
2.1.4 Dondoo ya Picha Na. 1 ........................................... Ukurasa 11
2.1.5 Kisa – Mkasa cha Wakala wa Koboko ............. Ukurasa 12
2.1.6 Dondoo kuhusu Kisa – Mkasa ......................... –“-
2.1.7 Dondoo ya Picha Na. 2 ........................................... Ukurasa 13
2.1.8 Dondoo za Mada ........................................... Ukurasa 14
2.1.9 Dondoo za Picha Na. 3 ........................................... Ukurasa 15

2.2 **Mada ya Pili:** Namna ya kudhibiti VVU na UKIMWI ..... **Ukurasa 16**
2.2.1 Dondoo ya Picha Na. 4 ........................................... –“-
2.2.2 Malengo Mahususi ........................................... –“-
2.2.3 Maudhui ........................................... –“-
2.2.4 Shughuli Mahususi ........................................... Ukurasa 17
2.2.5 Dondoo ya Picha Na. 5 ........................................... –“-
2.2.6 Ukubwa wa Tatizo la VVU na UKIMWI ............... Ukurasa 18
2.2.7 Dondoo za Mada ........................................... Ukurasa 19
2.2.8 Dondoo ya Picha Na. 6 ........................................... Ukurasa 20

2.3 **Mada ya Tatu:** Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza (MSY).. **Ukurasa 20**
2.3.1 Malengo Mahususi ........................................... –“-
2.3.2 Maudhui ........................................... Ukurasa 21
2.3.3 Shughuli Mahususi ........................................... –“-
2.3.4 Dondoo za Mada ........................................... –“-
a) Maana ya MSY ........................................... –“-
b) Aina za MSY ........................................... –“-
c) Mambo ya Kuzingatia na kuepuka .......................... Ukurasa 22
d) Umuhimu wa kufanya tathmini ya MSY .................. Ukurasa 23

**3.0 Sehemu C ........................................................................ Ukurasa 24**

3.1 **Mada ya Kwanza:** Fursa na Haki za Mtumishi ............. **Ukurasa 24**
3.1.2 Malengo Mahususi ................................................ –“-
3.1.3 Maudhui ................................................................ –“-
3.1.4 Shughuli Mahususi ............................................... –“-
3.1.5 Dondoo ya Picha Na. 7 ........................................ Ukurasa 25
3.1.6 Dondoo ya Mada ................................................. Ukurasa 26
3.1.7 Maana ya Unyanyapaa na Ubaguzi .................... –“-
3.1.8 Dondoo ya Mada ................................................ Ukurasa 27

3.2 **Mada ya Pili:** Muundo na Wajibu wa Kamati za VVU, UKIMWI na MSY Mahali pa Kazi ............................ **Ukurasa 27**
3.2.1 Malengo Mahususi ............................................. –“-
3.2.2 Maudhui ............................................................. –“-
3.2.3 Shughuli Mahususi ........................................... –“-
3.2.4 Dondoo ya Picha Na. 8 ..................................... Ukurasa 28
3.2.5 Dondoo za Mada .............................................. –“-

3.3 **Mada ya Tatu:** Mpango Kazi ...................................... **Ukurasa 30**
3.3.1 Malengo Mahususi ............................................ –“-
3.3.2 Maudhui ............................................................ –“-
3.3.3 Shughuli Mahususi ........................................... –“-
3.3.4 Dondoo za Mada .............................................. Ukurasa 31
3.3.5 Mambo ya Kuzingatia katika kufanya Tathmini .. –“-
3.3.6 Dondoo Muhimu ................................................ Ukurasa 32
3.3.7 Mafunzo na Gharama ........................................ –“-

3.4 **Mada ya Nne:** Ufuatiliaji, Tathmini na Taarifa ya Utekelezaji ... **Ukurasa 32**
3.4.1 Malengo Mahususi ............................................................ –“-
3.4.2 Maudhui ............................................................................ Ukurasa 33
3.4.3 Shughuli Mahususi .......................................................... –“-
3.4.4 Dondoo za Mada ............................................................. –“-

## MAENEO YA KITINI

Kitini hiki kimegawanyika katika maeneo makuu matatu, yenye sehemu A, B na C.

**Sehemu A** - inatoa maelezo ya utangulizi, madhumuni, mbinu za uwezeshaji, vifaa vitakavyotumika wakati wa uwezeshaji na muda wa mafunzo.

**Sehemu B** – inatoa maelezo kuhusu Umuhimu wa Kudhibiti VVU na UKIMWI katika Utumishi wa Umma, Namna ya kudhibiti VVU na UKIMWI Mahali pa Kazi na Magonjwa Sugu Yasiyoambukizwa.

**Sehemu C** - inatoa maelezo kuhusu Fursa na Haki za Mtumishi wa Umma, Muundo na wajibu wa kamati za VVU, UKIMWI na MSY mahali pa kazi, Mpango Kazi, Ufuatiliaji, Tathmini, na Taarifa za Utekelezaji.

## 1.0 SEHEMU A

## 1.1 UTANGULIZI

Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma (OR-MUU) imekuwa msitari wa mbele Kuchukua hatua mbalimbali za mwitikio dhidi ya Masuala yanayohusu VVU, UKIMWI na MSY.

Katika mwaka 2014, Ofisi iliandaa mwongozo wa kudhibiti VU, UKIMWI na MSY Mahali pa katika Utumishi wa Umma. Dhamira ya mwongozo huo ni kulinda na kuimarisha afya na ustawi wa Watumishi wa Umma ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi wakati wote.

Katika kufanikisha dhamira hiyo, OR-MUU iliona umuhimu wa kuandaa kitini kitakachowezesha kutoa mafunzo ya utekelezaji wa mwongozo. Kitini hiki kinatafsiri Mwongozo katika lugha rahisi na kutoa elimu inayofanana kwa watumishi wote wa Umma. Hivyo basi kila mwezeshaji/mratibu atakayetoa elimu ya VVU, UKIMWI na MSY anapaswa kuzingatia maelekezo yaliyomo katika Kitini hiki.

Mtiririko wa mada zilizopo na ufafanuzi wake umezingatia mahitaji ya watumishi wa umma kutokana na mapendekezo mbalimbali yaliyokuwa yametolewa, aidha kitini hiki kitaongeza ufanisi katika utekelezaji wa shughuli za VVU, UKIMWI na MSY mahali pa kazi kwa kuzingatia Sera, Sheria, Kanuni na Taratibu zilizoainishwa katika mwongozo wa kudhibiti VVU, UKIMWI na MSY mahali pa kazi katika Utumishi wa Umma.

## 1.2 MADHUMUNI

Madhumuni ya Kitini hiki ni kumwongoza mwezeshaji kutoa elimu ya utekelezaji wa Mwongozo wa VVU, UKIMWI na MSY Mahali pa Kazi katika Utumishi wa Umma Ili watumishi waweze kuwa na uelewa kuhusu mwongozo huo na hatimaye kuchochea mabadiliko ya tabia yatakayoongeza tija mahali pa kazi.

## 1.3 MBINU ZA UWEZESHAJI

Uwasilishaji wa mada zilizomo katika Kitini hiki utahusisha Mihadhara; Kazi za Vikundi; Kisa Mkasa; Majadiliano; Uchunguzi kifani pamoja na Maswali na majibu. Kila mwanzo wa mada kuna malengo mahususi, maudhui na shughuli mahususi.

## 1.4 VIFAA VITAKAVYO TUMIKA

Bango kitita, marker pen, kompyuta mpakato (Lap top), projecta ,ubao, kadi za manilla (kadi ngumu) na shajala

## 1.5 MUDA WA MAFUNZO

Ili washiriki waweze kuelewa vizuri utekelezaji wa Mwongozo wa kudhibiti VVU, UKIMWI na MSY mahali pa kazi katika Utumishi wa Umma, Kitini hiki kitafundishwa kwa kuzingatia maeneo yote kwa muda wa siku tatu. Hivyo mwezeshaji anatakiwa kuzingatia maagizo haya.

## 2.0 SEHEMU B

Sehemu hii mwezeshaji atatoa elimu kuhusu - Umuhimu wa Kudhibiti VVU na UKIMWI katika Utumishi wa Umma, Namna ya kudhibiti VVU na UKIMWI Mahali pa Kazi na Magonjwa Sugu Yasiyoambukizwa.

## 2.1 MADA YA KWANZA: Umuhimu wa kudhibiti VVU na UKIMWI katika utumishi wa Umma

### 2.1.1 Malengo Mahususi: Kuwawezesha washiriki:-

a) Kufahamu dhana ya VVU na UKIMWI
b) Kujua madhara ya VVU na UKIMWI mahali pa kazi
c) Kuelewa uhusiano baina ya mtindo wa maisha na VVU na UKIMWI
d) Kujua vichocheo vya maambukizi ya VVU
e) Kuelewa umuhimu wa kudhibiti VVU na UKIMWI mahali pa kazi
f) Kufahamu hatua za kudhibiti VVU na UKIMWI mahali pa kazi


### 2.1.2 Maudhui:

a) Maambukizi ya VVU
b) Matibabu na huduma kwa watumishi wanaoishi na VVU (WAVIU)
c) Umuhimu wa kupima na kujikinga na VVU
d) Umuhimu wa kujua hali halisi kabla ya kuanza udhibiti wa VVU na UKIMWI mahali pa kazi

### 2.1.3 Shughuli Mahususi:

a) Mwezeshaji awadodose washiriki kuhusu uelewa na matarajio yao juu ya udhibiti wa VVU na UKIMWI
b) Mwezeshaji agawe washiriki katika makundi.
c) Washiriki wafanye zoezi katika kisa mkasa cha wakala wa KOBOKO.

**2.1.4 Dondoo ya picha na 1 -** Inaonyesha tofauti baina ya Mtu mwenye VVU na UKIMWI




**2.1.5 Kisa-Mkasa cha Wakala wa Koboko:**

Hali Halisi ya Utoaji wa Huduma katika Wakala wa Koboko - *Wakala wa kiboko ni moja ya Wakala za Serikali ambayo ina changia pato la Taifa kutokana na umuhimu wa huduma wanayotoa kwa umma. Wakala ina jumla ya watumishi mia moja (100) ambao ni viongozi (menejimenti), wataalam (wahandisi, wachumi, wahasibu, maafisa tawala, wajiolojia) na watumishi wasaidizi.*

*Katika mwaka wa fedha 2013/14 Wakala iliendesha zoezi la upimaji wa afya za watumishi wake kwa ajili ya kuandaa mpango wa ustawi wa afya za watumishi. Matokeo ya upimaji yalionesha kuwa jumla ya watumishi kumi na wanane (18) wana maambukizi ya VVU, ambao 12 ni wataalam na 6 ni watumishi wasaidizi. Baada ya Mtendaji Mkuu kupata matokeo hayo alimwita Mkuu wa Idara ya Rasilimali watu ili kushauriana kuhusu hatua za kuchukua katika kudhibiti maambukizi mapya ya VVU na kuwahudumia watumishi waliobainika kuwa na maambukizi ya VVU.*

**2.1.6 Mwezeshaji awadodose washiriki kuhusu:**

i. Umuhimu wa kupima Afya za watumishi
ii. Madhara ya matokeo hayo katika nguvu kazi ya wakala wa Koboko
iii. Athari za matokeo hayo katika utekelezaji wa majukumu ya wakala wa KOBOKO
iv. Hatua zinazopaswa kuchukuliwa na uongozi wa Wakala wa Koboko
v. Changamoto zitakazokabili wakala huu katika kupata suluhisho dhidi ya matokeo hayo

d) Washiriki wawasilishe mrejesho wa zoezi kwa kila kikundi.
e) Mwezeshaji atoe majumuisho.
f) Mwezeshaji aeleze umuhimu wa kudhibiti VVU na UKIMWI katika utumishi wa umma kwa kuzingatia mtiririko ufuatao:-

- Hali halisi
- Madhara
- Uhusiano baina ya mtindo wa maisha na VVU na UKIMWI
- Vichocheo vinavyosababisha VVU na UKIMWI
- Hatua za VVU na UKIMWI
- Njia za kudhibiti VVU na UKIMWI

**Picha 2**



Mwezeshaji awaulize washiriki maoni yao kuhusiana na picha Na. 2

**2.1.7 Dondoo za picha Na. 2**

- Mwezeshaji awafafanulie washiriki kuhusu picha namba 2 kuwa huyo ni mwajiri ambaye anampokea mtumishi mahali pa kazi na anaonesha dalili za kumtamani kimapenzi.
- Mwajiri anaonesha kuwa ni mzembe katika kutimiza majukumu yake kwani mafaili ni mengi mezani kwake ambayo hayajafanyiwa kazi.
- Uwezekano wa uwepo wa rushwa ya ngono umetawala katika picha hii.
- Washiriki waulizwe uwepo wa vitendo hivyo katika Taasisi zao, na wabainishe hatua zinazochukuliwa katika kukabiliana nazo.
- Matumizi mabaya ya madaraka na ofisi, kinyume na maadili ya Utumishi.

**2.1.8 Dondoo za mada -** Mwezeshaji awaeleze washiriki masuala yafuatayo:-

| Sn | Mada | Dondoo |
|---|---|---|
| 1. | Maambukizi ya VVU | • Kuepuka maambukizi ni vema kuzingatia dhana ya ABCDE (A - Acha kabisa kujamiana, B- Bakia na Mpenzi asiye na maambukizi,C - Condom ikitumika kwa usahihi na wakati wote, D - Disclosure (kuwa wazi) E - Empowerment (Kuwa na ujasiri wa Maamuzi)<br>• Kuzuia Magonjwa ya Ngono<br>• Hamasa kwa watumishi kuhusu mikakati ya kuzuia VVU<br>• Kushawishi watumishi Kupewa Unasihi kupima VVU<br>• Kutokomeza Maambukizi kutoka kwa Mama kwenda kwa Mtoto. |
| 2. | Matibabu na huduma kwa watumishi wanaoishi na VVU (WAVIU) | • Watumishi wasisitizwe umuhimu wa kuhakikisha wanamiliki kadi ya uanachama wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF).<br>• Hamasa itolewe kwa watumishi wote ambao watagundulika kuishi na VVU kupata huduma za kitabibu.<br>• Mtumishi mwenye kuishi na VVU ambaye kiwango chake cha kinga ya mwili (CD4) kipo chini ya **350** anatakiwa kuanzishiwa dawa za kufubaza makali ya VVU (ARVs).<br>• Mtumishi mwenye VVU ahimizwe kufahamu na kuutumia Waraka Na. 2 wa VVU, UKIMWI na MSY wa Oktoba, 2014 kuhusu huduma zitolewazo kwa WAVIU. |
| 3. | Umuhimu wa kupima na kujikinga na VVU | • Uwepo wa watumishi wanaomudu majukumu yao na kuongeza tija<br>• Mwajiri kuweka mipango inayolingana na mahitaji halisi ya watumishi wa taasisi husika<br>• Watumishi na waajiri wahamasishwe umuhimu wa kupima VVU kwa hiari<br>• Watumishi wahamasishwe kujiweka wazi juu ya hali yao ya VVU ili waweze kupatiwa huduma kwa mujibu Waraka wa kudhibiti VVU , UKIMWI na MSY katika utumishi wa uma Na. 2 wa October 2014. Uhamasishaji huo usiwe wa lazima<br>• Watumishi waelimishwe umuhimu wa kufikia sifuri TATU (maambukizi mapya sifuri, unyanyapaa sifuri na vifo sifuri).<br>• Mwajiri analazimika kutunza siri na nyaraka za watumishi kuhusiana na hali ya VVU.<br>• Upimaji isiwe ni kigezo cha mtumishi kupata ajira, kupanda cheo au kwenda kwenye mafunzo.<br>• Watumishi wahimizwe kuchukua njia stahiki Kuepuka maambukizi mapya ya VVU |
| 4. | Umuhimu wa kujua hali halisi kabla ya kuanza udhibiti wa | • Kupata taarifa sahihi kabla ya kuanza utekelezaji wa Afua za VVU na UKIMWI mahali pa kazi<br>• Kuweza kupanga mipango yenye kuendana na hali halisi ya |

| Sn | Mada | Dondoo |
|---|---|---|
| | VVU na UKIMWI mahali pa kazi | taasisi<br>• Kupata mahitaji halisi ya rasilimali zinazohitajika |

**Picha 3**




### 2.1.9 Dondoo za picha Na. 3

- Inaonesha uwezekano wa Mteja/Mgonjwa kuwa na aina ya ugonjwa unaoambukiza kwa njia ya kufanya Ngono zembe.
- Mteja/Mgonjwa anamahusiano ya kimapenzi na zaidi ya mtu mmoja (Mchepukaji).
- Mteja/Mgonjwa anapata kigugumizi cha jinsi ya kuwataarifu wapenzi wake kutokana na unyanyapaa binafsi.
- Mtoa huduma yupo makini na utendaji wake wa kazi

## 2.2 MADA YA PILI: Namna ya Kudhibiti VVU na UKIMWI, Mahali pa Kazi

**Picha 4**




Mwezeshaji awaulize washiriki maoni yao kuhusiana na picha Na. 4

**2.2.1 Dondoo ya picha Na 4**

- Mahali pa kazi watumishi wenye madaraka hutumia madaraka yao kuomba rushwa ya ngono kwa watumishi wenzao.
- Mtumishi wa kike anaonesha ujasiri wa kufanya maamuzi na msimamo.
- Mtumishi wa kike anaelewa madhara ya mchepuko.

**2.2.2 Malengo Mahususi -** Kuwawezesha washiriki:-

a) Kuelewa juu ya udhibiti wa VVU na UKIMWI mahali pa kazi.
b) Kufahamu wajibu wa Mwajiri na Mtumishi katika udhibiti wa VVU na UKIMWI mahali pa kazi.
c) Kuelewa njia na hatua za kudhibiti VVU na UKIMWI

**2.2.3 Maudhui:-**


a) Ukubwa wa tatizo la VVU na UKIMWI
b) Makundi yaliyo katika hatari ya maambukizi ya VVU
c) Huduma ya unasihi na kupima VVU

**2.2.4 Shughuli Mahususi:-**

a) Mwezeshaji aibue mjadala kuhusu uelewa na matarajio ya washiriki juu ya namna ya kudhibiti VVU na UKIMWI mahali pa kazi.

b) Mwezeshaji agawe washiriki katika vikundi ili waainishe njia na hatua za namna ya kudhibiti VVU na UKIMWi mahali pa kazi.
c) Uwasilishaji wa kazi za vikundi.
d) Mwezeshaji aeleze namna ya kudhibiti VVU na UKIMWI katika utumishi wa umma kwa kuzingatia mtiririko ufuatao:-
   - Ukubwa wa tatizo la VVU na UKIMWI
   - Makundi yaliyo katika hatari ya maambukizi ya VVU
   - huduma ya unasihi na kupima VVU
   - Wadau muhimu katika udhibiti wa VVU na UKIMWI

**Picha 5**





Washiriki wafanye bungua bongo kuhusiana na picha Na. 5

### 2.2.5 Dondoo ya picha Na. 5

- Ngono salama hufanyika kwa matumizi sahihi ya kondomu.
- Wazo la matumizi ya kondomu limejitokeza baada ya kuanza ngono.
- Mwanaume anaonesha kujali matumizi ya kondom, wakati mwanamke anaonesha kutojali.
- Mwezeshaji awaelekeze washiriki juu ya matumizi sahihi ya Kondomu.

**2.2.6 Ukubwa wa tatizo la VVU na UKIMWI:**




**Chanzo:** THMIS, 2011/12

**2.2.7 Dondoo za mada:** Mwezeshaji anatakiwa

| Sn | Mada | Dondoo |
|---|---|---|
| 1. | Ukubwa wa tatizo la VVU na UKIMWI | • Suala la VVU na UKIMWI bado ni tatizo japokuwa ni zaidi ya robo karne sasa tangu ilipogundulika Ulimwenguni.<br>• Inakadiriwa kiasi cha watu milioni 2.1 Ulimwenguni walipata maambukizi mapya ya VVU, na jumla ya WAVIU milioni 34 Ulimwenguni (UNAIDS, 2013).<br>• Tathmini ya VVU na UKIMWI iliyofanyika Nchini 2012, imeonesha kiwango cha maambukizi ya VVU Nchini ni asilimia 5.1; ambapo jumla ya Mikoa 10 iligundulika kuwa na maambukizi zaidi ya kiwango cha Taifa, ambapo wanawake 62% na wanaume 47% walipimwa VVU na kupokea majibu (Rejea Taarifa ya THMIS, 2012 na Ramani ya Nchi hapo juu).<br>• Katika utumishi wa Umma takwimu zinaonesha kuwa taasisi 103 kati ya 280 (37%) zina watumishi 1,645 waliojiweka wazi kuwa wanaishi na VVU (OR-MUU, 2013) |
| 2. | Makundi yaliyo katika hatari ya maambukizi ya VVU | • Ni kundi lolote miongoni mwa jamii yetu wakiwemo watumishi, ambao kiwango cha maambukizi ya VVU ni asilimia 5 au zaidi, k.m. Watu wanaotumia dawa za kulevya kwa njia ya kujidunga sindano (PWIDs), Watu wanaofanya mapenzi kinyume cha maumbile (Anal sex), Watu wanaofanya kazi ya Ngono (SW), pamoja na makundi maalum kama vile wanawake, wasichana na watumishi ambao huwa wanahama hama (Migrants), n.k |
| 3. | Huduma ya unasihi na kupima VVU | • Watumishi wote wa umma wanastahili kupata taarifa sahihi kuhusu VVU na UKIMWI pamoja na afya bora, huduma ya unasihi, upimaji wa afya.<br>• Uzoefu unaonesha kuwa baadhi ya watumishi wanaoishi na VVU na UKIMWI wasipopata huduma ya unasihi kwa wakati muafaka huweza kufanya maamuzi yasiyo sahihi, mfano kuacha kazi bila kuzingatia taratibu za kazi.<br>• Mwajiri anawajibika kusimamia upatikanaji wa huduma ya unasihi na ushauri kwa watumishi wote. Aidha, inasisitizwa kuwa watumishi waliojiweka wazi kuhusu VVU na UKIMWI waendelee kupatiwa huduma hizo kama ilivyoainishwa kwenye mwongozo na waraka wa 2014. |

**Picha 6**




Washiriki watoe maoni yao kuhusiana na picha Na. 6

### 2.2.8 Dondoo ya picha Na. 6

- Watumishi wa ngazi ya chini wameridhika kwenda kupima baada ya kumuona Meneja wao amepima.
- Kuna uwezekano watumishi hawa wawili wakawa na mahusiano ya kimapenzi.
- Meneja anaonesha ametoka kupima akiwa na furaha bila shaka amekutwa hana maambukizi ya VVU kwa wakati huo – Angalizo: furaha hiyo inaweza ikachochea kwenda kufanya ngono zembe na kupata maambukizi ya VVU; au kumfanya abadili tabia na kuepukana na maambukizi mapya ya VVU; au bado majibu siyo sahihi endapo alipata maambukizi ndani ya miezi mitatu iliyopita.
- Meneja amefurahi kwa kutokukutwa na maambukizi ya VVU, Je amepima MSY? Kwani afya yake inaonesha kuwa ni mnene na ana kitambi kikubwa.

## 2.3 Mada ya Tatu: Magonjwa Sugu Yasiyoambukizwa (MSY)

**2.3.1 MALENGO MAHUSUSI -** Kuwawezesha washiriki:-

a) Kuelewa maana ya MSY.
b) Kuelewa hali halisi ya MSY katika Utumishi wa Umma.
c) Kuelewa umuhimu wa kupima afya na kujikinga na MSY
d) Kuelewa mitindo ya maisha inayosababisha MSY.
e) Kuelewa mtindo bora wa maisha ili kujikinga na MSY.

### 2.3.2 Maudhui:

a) Aina ya MSY
b) Mambo ya kuzingatia na kuepuka katika udhibiti wa MSY
c) Umuhimu wa kujua hali halisi ya MSY mahali pa kazi

### 2.3.3 Shughuli Mahususi:

a) Mwezeshaji awagawe washiriki katika vikundi.
b) Washiriki waainishe MSY na vyanzo vyake.
c) Uwasilishaji kazi za vikundi.
d) Mwezeshaji atoe majumuisho
e) Mwezeshaji aeleze umuhimu wa udhibiti wa MSY mahali pa kazi,
f) Mambo muhimu ya kuzingatia na kuepuka ili kudhibiti MSY mahali pa kazi (Rejea kiambatisho namba 2 cha Mwongozo wa kudhibiti VVU,UKIMWI na MSY mahali pa kazi, 2014)

### 2.3.4 Dondoo za Mada:

a) **Maana ya MSY:** Ni magonjwa sugu ambayo hayawezi kuambukizwa kutoka mtu mmoja kwenda kwa mwingine. Magonjwa haya husababishwa na mtindo wa maisha usiofaa, k.m. Mlo usiozingatia afya, ukosefu wa mazoezi ya kutosha, matumizi ya tumbaku, na matumizi ya pombe kuzidi kiasi.

**b)** Aina ya MSY ni kama ifuatavyo:

- Magonjwa ya Moyo na Mishipa ya damu;
- Kisukari;
- Saratani;
- Mfumo wa Hewa;
- Magonjwa ya Akili;
- Magonjwa sugu ya kurithi, Figo na Macho;
- Tezi ya Shingo, Tezi Dume, n.k.

c) **Mambo ya kuzingatia na kuepuka katika udhibiti wa MSY:** Jedwali hapo chini limeorodhesha masuala muhimu ya kuzingatia katika kudhibiti VVU, UKIMWI na MSY.

| Na. | Magonjwa | Mambo ya kuzingatia | Mambo ya kuepuka |
|---|---|---|---|
| 1. | Shinikizo kubwa la damu | • Kufuata ushauri wa daktari kwa kutumia dawa kulingana namaelekezo<br>• Kula mlo kamili angalau mara tatu kwa siku<br>• Kula mbogamboga na matunda kiasi cha kutosha<br>• Tumia nafaka zisizokobolewa na jamii ya kunde kwa wingi<br>• Kupima shinikizo la damu mara kwa mara | • Kula vyakula vyenye chumvi nyingi na vilivyosindikwa kwa chumvi na sukari, vyakula vyenye mafuta<br>• Punguza kiasi cha ulaji wa nyama na hasa nyama nyekundu |
| 2. | Kisukari | • Kufanya mazoezi ya mwili angalau dakika 30 kila siku<br>• Kupima sukari mara kwa mara na kuzingatia ushauri wa daktari<br>• Kula matunda halisi kwa kiasi kidogo<br>• Kula vitunguu saumu na kunywa maji mengi | • Unywaji pombe<br>• Matumizi ya sigara na tumbaku<br>• Kupata msongo mwitu<br>• Kupata majeraha |
| 3. | Mfumo wa Hewa | • Kuzingatia ushauri wa daktari na kanuni bora za mtindo wa maisha<br>• Usafi wa mazingira ya nyumba na vyumba yenye madirisha makubwa<br>• Kuzingatia matumizi sahihi ya Viyoyozi<br>• Kula mlo kamili<br>• Kula milo midogo midogo mara kwa mara<br>• Kufanya mazoezi ya mwili<br>• Kula vyakula vya makapimlo kwa wingi | • Unywaji pombe<br>• Vumbi<br>• Barafu<br>• Harufu<br>• Punguza matumizi ya chumvi<br>• Punguza uzito au unene uliozidi |
| 4. | Saratani | • Kuzingatia ushauri wa daktari na kanuni bora za mtindo wa maisha<br>• Kufanya mazoezi ya mwili<br>• Kupima afya mara kwa mara | • Kula vyakula vyenye nishati lishe kwa wingi<br>• Kula nyama nyekundu<br>• Kula vyakula vilivyosindikwa<br>• Unywaji pombe na uvutaji sigara |
| 5. | Moyo | • Kutumia mafuta kiasi kidogo | • Mafuta yatokanayo na |

| Na. | Magonjwa | Mambo ya kuzingatia | Mambo ya kuepuka |
|---|---|---|---|
| | | • Punguza ulaji wa nyama (isizidi nusu kilo kwa juma)<br>• Ongeza matumizi ya nafaka hasa zisizokobolewa<br>• Kufanya mazoezi ya mwili angalau dakika 30 kwa siku. | wanyama (Jibini, ngozi ya kuku, siagi)<br>• Nyama nyekundu<br>• Uzito uliozidi<br>• Uvutaji sigara na tumbaku |
| 6. | VVU na UKIMWI | • Kupima afya mara kwa mara<br>• Kuzingatia ushauri wa daktari<br>• Kula mlo kamili ili kujenga afya bora<br>• Kukuza stadi za maisha – kujitambua, kujithamini na kufanya uamuzi sahihi. | • Kuepuka kuwa na mpenzi Zaidi ya mmoja<br>• Unywaji wa pombe kupindukia na utumiaji wa dawa za kulevya<br>• Ngono zembe |

d) **Umuhimu wa kujua hali halisi ya MSY mahali pa kazi -** Mwezeshaiji anatakiwa:

i. Kuwaelimisha washiriki kuelewa umuhimu wa kufanya tafiti dhidi ya masuala ya MSY katika eneo lao la kazi, ili hatimaye mwajiri aweze kupanga mahitaji halisi ya taasisi

ii. Ili kujua tathmini ya hali halisi ya MSY mahali pa kazi mambo yafuatayo yanatakiwa kuzingatiwa:

- Makundi yaliyo katika hatari ya kupata MSY;
- Takwimu kuhusu watumishi wanaoishi na MSY (jinsi na umri);
- Vichocheo vinavyosababisha kuongezeka kwa MSY;
- Uelewa wa nyaraka zinazohusu MSY;
- Mafunzo kuhusu udhibiti wa MSY yaliyotolewa katika kipindi husika;
- Bajeti iliyotengwa na kutolewa kwa ajili ya afua za MSY mahali pa kazi;
- Uwepo wa Kamati za VVU, UKIMWI na MSY mahali pa kazi;
- Uwepo wa huduma za kudhibiti MSY mahali pa kazi (Kifaa cha kupima shinikizo la damu, rula ya kupima urefu/kimo, mzani wa kupima uzito, kifaa cha kupima sukari, na vipeperushi na unasihi); na
- Uwepo wa uangalizi wa karibu unaojali afya na ustawi wa watumishi wa Umma mahali pa kazi (huduma ya unasihi, muda wa kupumzika na kazi nyepesi).

## 3.0 SEHEMU C

Sehemu hii mwezeshaji atatoa elimu kuhusu Fursa na Haki za Mtumishi wa Umma, Muundo na Wajibu wa Kamati za VVU, UKIMWI na MSY, Mpango Kazi, Ufuatiliaji, Tathmini na Taarifa za Utekelezaji, Mahali pa Kazi.

**3.1 MADA YA KWANZA:** Fursa na Haki za Mtumishi wa Umma

**3.1.2 Malengo Mahususi -** Kuwawezesha washiriki:-

a) Kuelewa maana ya fursa katika utumishi wa Umma.
b) Kubainisha fursa zilizopo kwa ajili ya mtumishi wa umma mahali pa kazi.
c) Kuelewa umuhimu wa fursa zilizopo na kuzitumia.
d) Kuelewa namna ya kuepuka Unyanyapaa na Ubaguzi.
e) Kuelewa umuhimu wa Unasihi.

**3.1.3 Maudhui:**

a) Fursa za watumishi wa umma
b) Haki na wajibu kwa watumishi wa umma mahali pa kazi
c) Unyanyapaa na Ubaguzi.
d) Huduma ya ushauri nasaha.

**3.1.4 Shughuli Mahususi:**

a) Mwezeshaji aeleze fursa za watumishi zilizotajwa katika Waraka No. 2 wa huduma kwa watumishi wanaoishi na VVU, UKIMWI na MSY wa February 2014, pamoja na mwongozo wake.
b) Mwezeshaji agawe washiriki katika makundi.
c) Katika vikundi washiriki wataje uelewa wao kuhusu fursa wanazozifahamu, haki na wajibu kwa watumishi wa umma mahali pa kazi, na aina ya Unyanyapaa na Ubaguzi unaotokea katika taasisi zao.
d) Uwasilishaji wa kazi za vikundi ni kwa kila kikundi.
e) Mwezeshaji afanye majumuisho ya kazi za vikundi.
f) Mwezeshaji awafafanulie washiriki maana ya Unyanyapaa na Ubaguzi

**Picha 7**




Washiriki watoe maoni kuhusiana na picha Na. 7

**3.1.5 Dondoo ya picha Na. 7**

- Inaonesha watumishi wanaongelea suala la VVU na UKIMWI wakiwa kwenye kikao cha kazi.
- Unyanyapaa unapungua miongoni mwa watumishi – *“usijali, hapa haiwezi kuathiri kazi yako”*.
- Suala la Jinsia limezingatiwa.
- Kila mshiriki anaonesha kushiriki kikamilifu.

**3.1.6 Dondoo za mada:** Fursa za Watumishi wa Umma

| Sn | Mada | Dondoo |
|---|---|---|
| 1. | Fursa na haki za watumishi wa umma | • Watumishi wa Umma wana fursa mbali mbali mahali pa kazi kama zinavyoainishwa katika nyaraka mbalimbali za Serikali ikiwemo mwongozo wa VVU, UKIMWI na MSY Mahali pa Kazi (2014).<br>• Kila mtumishi anastahili kupewa haki mahali pa kazi kulingana na sheria, kanuni, taratibu na masharti ya ajira yake;<br>• Watumishi wa umma wasinyanyapaliwe wala kubaguliwa kwa vigezo tu kwamba ana VVU, UKIMWI au MSY.<br>• Vilevile ana Haki ya kupata huduma ya Unasihi na Ushauri. Hivyo inaelekezwa kuwa Waajiri katika Utumishi wa Umma waweke mazingira wezeshi ya upatikanaji wa nyaraka hizi na Watumishi wana haki ya kupata nyaraka hizo, kuzisoma na kuzifanyia kazi. |
| 2. | Mwezeshaji afanye marejeo katika nyaraka zifuatazo:<br>• Mwongozo wa VVU, UKIMWI na MSY mahali pa Kazi katika Utumishi wa Umma, 2014 – www.utumishi.go.tz<br>• Sheria ya UKIMWI, 2008 – www.tacaids.go.tz<br>• Pendekezo kuhusu VVU na UKIMWI na Ulimwengu wa Kazi – 2010 (Na. 200) – www.ilo.org<br>• Kanuni kuhusu VVU na UKIMWI katika Ulimwengu wa Kazi, 2001 - www.ilo.org | |

### 3.1.7 Maana ya Unyanyapaa na Ubaguzi

Washiriki wakae katika makundi mawili, moja lijadili kuhusu Ubaguzi na lingine lijadili kuhusu Unyanyapaa kwa kuangalia picha hii



Mwezeshaji ahitimishe kuwa:

**Unyanyapaa** ---Mtazamo

**Ubaguzi** ----------Kitendo

Pia asisitize kuwa ni kinyume cha sheria kumbagua au kumnyanyapaa mfanyakazi/mtumishi wakati wa kutafuta kazi au akiwa kazini kwa kigezo tu kuwa mfanyakazi huyo anahisiwa kuwa ana VVU au anaishi na VVU

### 3.1.8 Dondoo za Mada: Unyanyapaa na Ubaguzi

| Sn | Mada | Dondoo |
|---|---|---|
| | Unyanyapaa na Ubaguzi | • **Unyanyapaa** ni kuwapachika watu sifa mbaya kutokana na ubainifu fulani kama jinsi, rangi, maradhi n.k.<br>• **Ubaguzi** ni kitendo kinachotokana na unyanyapaa. Kwa mfano, kumfanyia mtu ubaya kwamba hapaswi kuheshimiwa au kutokuwa na maana mbele za watu wengine.<br>• ***Unyanyapaa ni mtizamo na ubaguzi ni kitendo.***Unyanyapaa na ubaguzi una madhara makubwa. Kwa mfano kumbagua mtu anayeishi na Virusi Vya UKIMWI |

## 3.2 MADA YA PILI: Muundo na Wajibu wa Kamati za VVU, UKIMWI na MSY Mahali pa Kazi

### 2.3.1 Malengo Mahususi - Kuwawezesha washiriki:-

a) Kuelewa muundo na wajibu wa kamati za VVU, UKIMWI na MSY mahali pa kazi.
b) Kuelewa sifa na vigezo vya wajumbe wa kamati za VVU, UKIMWI na MSY.
c) Kuelewa maana ya Elimu Rika, sifa na majukumu ya Waelimisha rika Mahali pa kazi.

### 3.2.2 Maudhui:


a) Muundo na wajibu wa kamati
b) Umuhimu wa wajumbe walioteuliwa katika kamati/sifa na vigezo
c) Elimu rika mahali pa kazi,muelimisha rika mahali pa kazi na majukumu ya muelimisha rika

### 3.2.3 Shughuli Mahususi:

a) Mwezeshaji awaeleze washiriki kuhusu muundo wa kamati ya VVU, UKIMWI na MSY kama ilivyo kwenye Mwongozo wa kudhibiti VVU, UKIMWI na MSY mahali pa Kazi, 2014.
b) Mwezeshaji aainishe aina za kamati na majukumu yake katika ngazi ya Taifa, Wizara, Taasisi, Mkoa, Wilaya au Halmashauri (Msisitizo uwekwe katika ngazi ya washiriki).

c) Mwezeshaji awaalike washiriki kuelezea hali halisi kuhusu kamati ya VVU, UKIMWI na MSY mahali pa kazi
d) Mwezeshaji awaulize washiriki wanaelewa nini kuhusiana na dhana ya Elimu Rika
e) Mwezeshaji awaalike washiriki kutoa uzoefu wao kuhusu namna wanavyoelimisha masuala ya VVU, UKIMWI na MSY mahali pa kazi
f) Mwezeshaji atoe majumuisho kulingana na mada na uzoefu kutoka kwa washiriki.

**Picha 8**




Washiriki watoe maoni kuhusiana na picha Na. 8

### 3.2.4 Dondoo ya picha Na. 8

- Inaonesha kuwa muelimshajirika anaweza kuwa yeyote miongoni mwa watumishi
- Inaonesha kuwa uelimishajirika haujalishi jinsi ya mtumishi.
- Umuhimu wa muelimishajirika mahali pa kazi.

**3.2.5 Dondoo za Mada:** Mwezeshaji afafanue kwa kina yafuatayo:-

| Sn | Mada | Dondoo |
|---|---|---|
| 1. | Muundo na wajibu wa kamati | • Washiriki waelimishwe juu ya kamati za VVU, UKIMWI na MSY mahali pakazi<br>• Majukumu ya kila kamati katika kila ngazi kama ilivyoainishwa katika Mwongozo wa VVU, UKIMWI na MSY Mahali pa Kazi. |

| Sn | Mada | Dondoo |
| --- | --- | --- |
| | | • Pia afafanue vigezo vya uteuzi wa wajumbe wa kamati. |
| 2. | Mwongozo huu pia unaelezea uwepo wa waratibu na waelimishaji rika wa VVU, UKIMWI na MSY mahali pa Kazi na kuainisha majukumu yao. | • Kuandaa mpango kazi kwa kushirikisha kamati ya VVU, UKIMWI na MSY mahali pa kazi,<br>• Kusimamia na kuratibu utekelezaji wa afua za VVU, UKIMWI na MSY mahali pa kazi,<br>• Kukusanya, kuchambua, kutumia na kutunza takwimu za afua za VVU, UKIMWI na MSY mahali pa kazi,<br>• Kuratibu uandaaji wa taarifa za utekelezaji wa afua za VVU, UKIMWI na MSY mahali pa kazi na kuziwasilisha kwenye Kamati,<br>• Kuwezesha mchakato wa upatikanaji wa waelimisha rika kwa kushirikisha kamati ya afua za VVU, UKIMWI na MSY mahali pa kazi,<br>• Kuratibu shughuli za waelimisha rika mahali pa kazi. |
| 3. | Sifa za mwelimisha rika. | • Awe ni mtumishi wa Umma;<br>• Awe ni mtumishi anayeweza kuongea mbele za watu kwa kujiamini na bila woga;<br>• Awe ni mtumishi anayeweza kutunza siri na kutoa ushauri kwa watumishi wenzake bila kuogopa;<br>• Awe tayari kupokea mawazo, maoni au ushauri toka kwa watumishi katika Idara/kitengo yake na kuwasilisha kwa mratibu wa VVU, UKIMWI na MSY mahali pa kazi;<br>• Awe mtumishi mwenye kuwajibika na kujituma katika masuala ya kijamii.<br>• Apatikane kwa uteuzi wa mkuu idara/kitengo husika kwa kuzingatia sifa na vigezo vilivyoainishwa |
| 4. | Vigezo muhimu vya wajumbe kama ifuatavyo; | • Mwenyekiti wa kamati atakuwa ni mtendaji mkuu wa taasisi, kwa sababu wao ndio wawajibikaji wakuu wa utekelezaji wa majukumu yote ya taasisi husika,<br>• Katibu wa kamati ni mkuu wa idara ya utawala na rasilimali watu, kwa sababu anasimamia maslahi ya watumishi walio chini yake hivyo ni rahisi kwake kujua mahitaji muhimu ya kamati ya VVU, UKIMWI na MSY.<br>• Katika taasisi nyingine anaweza kuwa mkuu wa idara /kitengo/sehemu inayosimamia rasilimali watu/katibu tawala msaidizi, utawala na rasilimamali watu/mkuu wa idara ya utumishi na rasilimaliwatu/ au na afisa maendeleo ya jamii wa kata. |

| Sn | Mada | Dondoo |
|---|---|---|
| | | • Mkuu wa idara ya mipango/katibu tawala msaidizi, mipango na uratibu/maafisa watendaji wa mitaa/vijiji katika kata husika wameteuliwa kuingia kwenye kamati ili kusimamia uingizaji wa afua za VVU, UKIMWI na MSY kwenye mipango ya taasisi husika wakati wa uaandaaji na utekelezaji wa bajeti.<br>• Mhasibu wa taasisi ni mjumbe wa kamati kwani yeye ndio msimamizi wa mgawanyo wa rasilimali fedha, atahakikisha fedha zilizotengwa kwa ajili ya VVU, UKIMWI na MSY hazitumiki kwa shughuli nyingine yoyote.<br>• Mratibu wa VVU,UKIMWI na MSY mahali pa kazi ndiye mshauri na mratibu wa utekelezaji wa mpango wa VVU,UKIMWI na MSY uliowekwa na taasisi.<br>• Mwakilishi wa WAVIU na wanaoishi na MSY ni msemaji na mwakilishi wa kundi lengwa ili kuhakikisha maslahi na vigezo vinazingatiwa.<br>• Mwakilishi wa chama cha wafanyakazi, katika taasisi husika ni msimamizi wa haki za wafanyakazi wote wakiwemo WAVIU na wanaoishi na MSY.<br>• Daktari wa binadamu, ili kutoa ushauri wa kitabibu katika kamati kwa ujumla.<br>• Mtaalam wa lishe anatoa ushauri kwenye kamati ya VVU, UKIMWI na MSY katika taasisi kuhusu masuala ya lishe. |

**3.3 MADA YA TATU:** Mpango Kazi

**3.3.1 Malengo ya Mahususi -** Kuwawezesha washiriki:--

a) Kuelewa maana ya mpango wa VVU, UKIMWI na MSY Mahali pa kazi
b) Kuelewa jinsi ya kuandaa mpango wa VVU, UKIMWI na MSY
c) Kuelewa kuainisha vyanzo vya rasilimali fedha katika taasisi zao.
d) Kutekeleza shughuli za VVU, UKIMWI na MSY kulingana na mpango wao.

**3.3.2 Maudhui:**

a) Ufafanuzi kuhusu dhana ya Mpango, Mafunzo na Bajeti
b) Umuhimu wa mpango Mahali pa kazi

**3.3.3 Shughuli Mahususi:**

a) Mwezeshaji awagawe washiriki katika makundi kulingana na idadi ya washiriki.
b) Washiriki waandae Mpango wa utekelezaji wa masuala ya VVU, UKIMWI na MSY.
c) Uwasilishaji kutoka kila makundi.
d) Mwezeshaji atoa majumuisho ya kazi za vikundi kulingana na mwongozo.
e) Mwezeshaji atoe mfano wa mpango kulingana na mwongozo.

f) Mwezeshaji aeleze kwa kifupi umuhimu wa mafunzo na bajeti kuhusu VVU, UKIMWI na MSY.

**3.3.4 Dondoo za Mada:** Mpango kazi utaandaliwa kwa kutumia taarifa ya tathmini ya awali ya hali halisi ya VVU, UKIMWI na MSY mahali pa kazi. Aidha mpango kazi huo uandaliwe kwa kushirikisha kamati ya VVU, UKIMWI na MSY mahali pa kazi.

**3.3.5 Mambo ya kuzingatia katika kufanya tathimini ya awali ya hali halisi:-**

- Makundi yaliyo katika hatari ya kupata MSY na kuambukizwa VVU;
- Takwimu kuhusu watumishi wanaoishi na VVU, UKIMWI na MSY (jinsi na umri);
- Vichocheo vinavyosababisha kuongezeka kwa MSY na maambukizo ya VVU;
- Uelewa wa nyaraka zinazohusu VVU, UKIMWI na MSY;
- Mafunzo kuhusu udhibiti wa VVU, UKIMWI na MSY yaliyotolewa katika kipindi husika;
- Bajeti iliyotengwa na kutolewa kwa ajili ya afua za VVU, UKIMWI na MSY mahali pa kazi;
- Uwepo wa Kamati za VVU, UKIMWI na MSY, mahali pa kazi;
- Uwepo wa huduma za kudhibiti MSY na maambukizo ya VVU mahali pa kazi (Kifaa cha kupima shinikizo la damu, rula ya kupima urefu/kimo, mzani wa kupima uzito, kifaa cha kupima sukari , kondomu na vipeperushi na unasihi); na
- Uwepo wa uangalizi wa karibu unaojali afya na ustawi wa watumishi wa Umma mahali pa kazi (huduma ya unasihi, muda wa kupumzika na kazi nyepesi). Itawekwa kwenye Waraka.

**3.3.6 Dondoo muhimu:**

Mwezeshaji aeleze washiriki maana ya mpango kazi na mambo ya kuzingatia katika uandaaji wa mpango kazi. Mpango kazi uandaliwe na watumishi kwa kushirikiana na menejiment na uoneshe lengo, shughuli, vyanzo vya rasilimali, gharama zikakazohitajika kipindi cha utekelezaji, wahusika na majukumu yao ya kazi na kwa kuzingatia kiambatisho na.6 katika mwongozo wa VVU, UKIMWI na MSY (2014)

***Kwa mfano:***

**Mpango Kazi wa Wizara XX**

| Na. | Lengo | Shughuli | Vyanzo vya Rasilimali Fedha | Kiasi (TZS) | Kipindi cha Utekelezaji | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Utekelezaji wa mwongozo wa VVU, UKIMWI na MSY katika wizara XX | Kutoa mafunzo kuhusu Mwongozo kwa kamati ya Wizara xx | Wizara – Lengo A (Objective) | 200,000 | Aprili – Machi 2015 | Mratibu wa VVU, UKIMWI na MSY |
| 2 | Kuwa na wafanyakazi wenye afya na kuleta tija mahali pa kazi | Kuhamasisha watumishi kupima VVU na MSY | Wizara – Lengo A (Objective) | 200,000 | Aprili – Disemba 2015 | Kamati ya VVU, UKIMWI na MSY ya wizara xx |

**MAFUNZO NA GHARAMA**

Mwezeshaji awaeleze washiriki juu ya wajibu wa mwajiri wa kuandaa program ya mafunzo yanayohusu VVU, UKIMWI na MSY mahali pa kazi na kutenga fedha kama ilivyoelekezwa katika mwongozo wa VVU, UKIMWI na MSY katika Utumishi wa Umma, (2014).

**3.4 MADA YA NNE:** Ufuatiliaji, Tathmini na Taarifa Za Utekelezaji

**3.4.1 Malengo ya Mada -** Kuwawezesha washiriki:-

a) Kujua umuhimu wa Kamati kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa mpango kazi wa masuala ya VVU, UKIMWI na MSY.

b) Kuelewa namna ya kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Afua za VVU, UKIMWI na MSY.
c) Kuwa na uwezo wa kuandaa tarifa za utekelezaji wa Afua za VVU, UKIMWI na MSY.
d) Kuelewa utaratibu wa kuandaa na kuwasilisha taarifa za utekelezaji afua za VVU, UKIMWI na MSY kwa kuzingatia mwongozo.

**3.4.2 Maudhui:**

a) Ufuatiliaji wa utekelezaji
b) Tathmini ya utekelezaji
c) Uandaaji wa taarifa za utekelezaji
d) Mtiririko wa uwasilishaji wa Taariifa

**3.4.3 Shughuli Mahususi:**

a) Mwezeshaji awaongoze washiriki kujadili umuhimu wa kufanya ufuatiliaji wa mara kwa mara, tathmini na kuandaa na kuwasilisha taarifa ya utekelezaji wa afua za VVU, UKIMWI na MSY.
b) Mwezeshaji aeleze washiriki kuhusu njia za kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa afua za VVU, UKIMWI na MSY mahali pa kazi.
c) Mwezeshaji aeleze changamoto zinazoweza kujitokeza wakati wa kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji na awaalike washiriki kubainisha mbinu za kukabiliana na changamoto za ufuatiliaji.
d) Mwezeshaji agawe na kuwapitisha washiriki katika fomu ya uaandaaji wa taarifa za utekelezaji wa Afua za VVU, UKIMWI na MSY kama ilivyo katika kiambatisho Na.5 cha Mwongozo wa kudhibiti VVU, UKIMWI na MSY mahali pa kazi katika utumishi wa umma (2014).
e) Mwezeshaji aeleze washiriki kuhusu vipindi vya uandaaji wa taarifa za utekelezaji kulingana na mwongozo wa kudhibiti VVU, UKIMWI na MSY Mahali Pa Kazi Katika Utumishi wa Umma (2014).
f) Mwezeshaji aeleze mtiririko wa utoaji na upokeaji wa taarifa za utekelezaji wa Afua za VVU, UKIMWI na MSY katika utumishi wa umma kama ilivyoelekezwa katika mwongozo wa kudhibiti VVU, UKIMWI na MSY Mahali Pa Kazi Katika Utumishi wa Umma (2014).
g) Vikundi viwasilishe taarifa zao.
h) Mwezeshaji afanye majumuisho ya mada.

**3.4.4 Dondoo za mada:** Mwezeshaji anatakiwa kufafanua kama ifuatavyo;-

| Sn | Mada | Dondoo |
|---|---|---|
| 1. | Ufuatiliaji wa utekelezaji | • Ufuatiliaji wa utekelezaji wa afua za VVU, UKIMWI na MSY kwa kushirikisha watumishi wa Taasisi ni muhimu kufanyika mara kwa mara ili kuweza kubaini changamoto zilizopo na kupata suluhisho.<br>• Mwajiri kupitia kamati husika anawajibika kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa Afua za VVU, UKIMWI na MSY |

| Sn | Mada | Dondoo |
|---|---|---|
| 2. | Tathmini ya utekelezaji | • Shughuli za VVU, UKIMWI na MSY mahali pa kazi utekelezaji wake hutathminiwa kwa kipindi cha muda mfupi na mrefu.<br>• Tathmini ya utekelezaji wa Afua hufanyika kila mwisho wa mwaka katika taasisi na taarifa zake hutumika kuboresha mipango kazi ya miaka inayofuata.<br>• Tathmini ya muda mrefu itafanywa na OR-MUU ili kuangalia hali ya utumishi wa Umma kwa ujumla wake. |
| 3. | Uandaaji wa taarifa za utekelezaji | Waajiri wote katika Utumishi wa Umma wanajukumu la kuandaa taarifa za utekelezaji wa Afua za VVU, UKIMWI na MSY kwa kila robo mwaka na kuziwasilisha OR-MUU na nakala TACAIDS kwa kuzingatia muundo wa taarifa uliopo katika Mwongozo wa VVU, UKIMWI na MSY, Februari, 2014 *(Kiambatisho Na. 5).* |
| 4. | Mtiririko wa uwasilishaji wa Taariifa | • Taasisi za Umma zinawajibu wa kuwasilisha taarifa za utekelezaji OR–MUU, na nakala TACAIDS kila robo mwaka.<br>• Aidha, Taasisi zitatakiwa kuwasilisha taarifa kwa mamlaka zao kama ilivyoelekezwa kwenye kipengele Na. 7.3.1 kilichopo kwenye mwongozo wa VVU, UKIMWI na MSY (Februari, 2014). |